TANGAZO LA SERIKALI Na. 1073 la tarehe 20/12/2024

SHERIA YA MISITU,

(SURA YA 323)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 29(1))*

NOTISI YA KUSUDIO LA KUTANGAZA MABADILIKO YA ENEO LA MSITU WA HIFADHI WA TAIFA NDECHELA YA MWAKA 2024

**KWA KUWA**, Eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa Ndechela lilitangazwa chini ya Tangazo la Serikali Na. 551 la Mwaka 1958 kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Ndechela;

**KWA KUWA**, Waziri kwa mamlaka aliyopewa chini ya Sheria ya Misitu, Sura ya 323 anaona kwamba ni kwa maslahi ya umma kufanya mabadiliko ya eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa Ndechela;

NA KWA KUWA, Waziri, kwa kuzingatia Sheria ya Misitu, Sura ya 323 ambayo, pamoja na masharti mengine inamtaka, anapokusudia kutangaza mabadiliko ya eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa, kutoa notisi ya kusudio kwa umma kabla ya kutekeleza mamlaka hayo;

**HIVYO BASI**, Waziri anatamka kama ifuatavyo:

Jina

**1**. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kusudio la Kutangaza Mabadiliko ya Msitu wa Hifadhi wa Taifa Ndechela ya Mwaka 2024.

Eneo linalopendekezwa kutangazwa

**2**. Eneo la hifadhi lililo ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali la Notisi hii linapendekezwa kutangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Ndechela.

Madhumuni ya tangazo

**3**. Madhumuni ya mabadiliko ya eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa Ndechela ni-

(a) kuondoa sehemu ya eneo la ardhi ya Msitu wa Hifadhi ya Taifa Ndechela ili kutatua migogoro ya ardhi; na

(b) kuhifadhi baioanuwai, vyanzo vya maji ili kuendeleza madhumuni ya usimamizi, uhifadhi wa eneo la msitu na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu katika eneo la msitu.

Uhalali wa Notisi

**4**.-(1) Notisi hii itakuwa halali kwa muda wa siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

(2) Ndani ya kipindi hicho cha siku tisini, mtu au kundi la watu au mwakilishi wao anaweza, kwa maandishi kuwasilisha pingamizi, maoni au madai ya haki yoyote inayotokana na sheria za kimila kuhusiana na ardhi au mazao ya msitu au haki yoyote iliyoainishwa kwenye sheria nyingine katika eneo la kutangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Ndechela ambalo linapendekezwa kubadilishwa.

Uwasilishaji wa pingamizi

**5**. Pingamizi, maoni au madai yoyote dhidi ya kusudio la kutangaza mabadiliko ya eneo la Msitu wa Hifadhi wa Taifa Ndechela yawasilishwe ndani ya siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa Notisi hii kwa anuani ifuatayo:

Katibu Mkuu,
Wizara ya Maliasili na Utalii,
S.L.P. 1351,
DODOMA.

*Tangazo la serikali Na.1073 (Linaendelea.)*


JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

WILAYA YA NANYUMBU
MSITU WA HIFADHI WA NDECHELA

Makadirio ya eneo: Hekta 7088.76 au Kilometa za Mraba 70.89 Unakopatikana na Mipaka:

Eneo lote la hifadhi awali chini ya Eneo la Msitu wa Hifadhi wa Ndechela linalopatikana Wilaya ya Nanyumbu, Mkoa wa Mtwara kama lilivyochorwa katika Ramani Na. Jb 2743 (Skeli 1:25,000) iliyohifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Upimaji na Ramani na lenye mipaka ifuatayo:




Dodoma
11th November, 2024

PINDI HAZARA CHANA,
*Waziri wa Maliasili na Utalii*